# TAARIFA YA UKUSANYAJI WA MAPATO YA NDANI YA HALMASHAURI KWA KIPINDI CHA NUSU MWAKA (JULAI – DESEMBA, 2019) KWA MWAKA WA FEDHA 2019/2020

## 1.0 Utangulizi

Ofisi ya Rais TAMISEMI ina utaratibu wa kutangaza taarifa za mapato ya ndani ya Halmashauri kila robo mwaka kwa Umma ili kuongeza uwazi na uwajibikaji katika ukusanyaji wa mapato ya ndani ya Halmashauri nchini. Aidha, utaratibu huu unawawezesha Viongozi katika ngazi za Mikoa kusimamia vyema Halmashauri zao ili ziweze kukusanya mapato ya kutosha kwa kuzingatia malengo ya bajeti zilizoidhinishwa.

Taarifa hii inalenga kuelezea ukusanyaji wa mapato ya vyanzo vya ndani vya Halmashauri kwa kipindi cha nusu mwaka (Julai – Desemba, 2019). Maelezo ya taarifa hii yameainisha makisio ya mwaka na mapato halisi ya kila Halmashauri, ufanisi wa ukusanyaji na wingi wa mapato hayo kwa kulinganisha aina za Halmashauri zilizowekwa katika makundi. Pia taarifa hii imeainisha matumizi ya kawaida, matumizi ya maendeleo ya fedha za ndani za Halmashauri pamoja na mikopo iliyotolewa kwa Wanawake, Vijana na Watu Wenye Ulemavu kwa kipindi cha Julai hadi Desemba, 2019.

### 1.1 Hali ya Ukusanyaji wa Mapato kwa Halmasahuri Zote

Kwa Mwaka wa Fedha 2019/20 Halmashauri zilipanga kukusanya **Shilingi Bilioni 765.48** kutoka kwenye vyanzo vyake vya ndani. Katika kipindi cha nusu mwaka (Julai hadi Desemba, 2019) Halmashauri zimekusanya Jumla ya **Shilingi bilioni 356.81** ambayo ni **asilimia 47** ya makisio ya mwaka.

Uchambuzi wa taarifa za mapato ya vyanzo vya ndani vya Halmashauri katika kipindi cha Julai - Desemba, 2019 umeonesha kuwepo kwa ongezeko la mapato yaliyokusanywa kwa kiasi cha **Shilingi bilioni 56.7** ikilinganishwa na kiasi kilichokusanywa katika kipindi kama hicho cha Julai - Desemba, 2018 sawa na ongezeko la **asilimia 19.**

Uchambuzi unaonesha kuwa katika kipindi cha Julai hadi Desemba, 2019 Halmashauri **63** kati ya Halmashauri **185** zimekusanya mapato ya ndani kwa **asilimia 50 na zaidi** ya makisio kwa Mwaka wa Fedha 2019/20. Aidha, Halmashauri **mia ishirini na mbili (122)** zimekusanya mapato ya ndani chini ya asilimia **50** ya makisio ya mwaka.

Aidha, Halmashauri hukusanya mapato mengi au kidogo kwenye vyanzo tofauti kulingana na hali halisi ya shughuli za kiuchumi za kila Halmashauri. Hivyo, ongezeko hilo limetokana na sababu mbalimbali ikiwemo ushuru wa zao la Korosho katika Halmashauri za Mikoa ya Mtwara na Lindi na Halmashauri ya Wilaya ya Tunduru Mkoa wa Ruvuma.

### 1.2 Ufanisi Katika Ukusanyaji Mapato

Katika kipindi cha miezi sita (Julai – Desemba, 2019), Halmashauri za Wilaya za **Tunduru na Kibondo** zimekusanya mapato kwa **asilimia 104** ya makisio ya mwaka 2019/2020. Halmashauri zote zilizokusanya zaidi ya asilimia 100 hadi Desemba, 2019 na zile ambazo zimejitathmini na kuona upo uwezekano wa kuzidi asilimia 100 ya bajeti za mapato ya ndani ifikapo Juni, 2020 zinaelekezwa kufanya mapitio ya Bajeti kwa mujibu wa **Sheria ya Bajeti ya mwaka 2015** ili ziweze kuongeza Bajeti za mapato na matumizi ya fedha hizo. Aidha, Halmashauri za Wilaya za **Mafia, Ukerewe na Gairo** zimekusanya **asilimia 18 tu** ya makisio yake kwa kipindi cha miezi sita, *(Jedwali Na. 1).*

Katika kuzipima Halmashauri zote kwa kigezo cha wingi wa mapato (pato ghafi), Halmashauri ya Jiji la **Dodoma** imekusanya mapato mengi zaidi kuliko Halmashauri zote kwa kukusanya **Shilingi Bilioni 29.75** na Halmashauri ya Wilaya ya **Bumbuli** imekusanya mapato kidogo kuliko Halmashauri zote kwa kukusanya **Shilingi Milioni 186.10.**
*(Jedwali Na. 2).*

## 2.0 Uchambuzi

Uchambuzi wa mwenendo wa ukusanyaji wa mapato ya ndani ya Halmashauri katika kipindi hiki unaonesha hali ya ukusanyaji wa mapato ya ndani kwa kulinganisha Halmashauri moja moja, makundi ya Halmashauri na mapato ya ndani baina ya Mikoa.

### 2.1 Taarifa ya Mapato ya Ndani ya Halmashauri Kimkoa kwa Kuzingatia Asilimia ya Makusanyo

Mkoa wa Geita umefanya vizuri katika ukusanyaji wa mapato ya ndani kwa kipindi cha Julai hadi Desemba, 2019 ambapo umekusanya wastani wa **asilimia 63** ya makisio ya Halmashauri za Mkoa huo. Aidha, Mkoa wa mwisho kwa kigezo hicho ni Mkoa wa Tanga ambao umekusanya wastani wa **asilimia 36** ya makisio ya mwaka ya Halmashauri za Mkoa huo *(Jedwali Na. 3).*

### 2.2 Mapato ya Ndani ya Halmashauri Kimkoa kwa Kuzingatia Wingi wa Mapato

Kwa kigezo cha wingi wa mapato, Mkoa wa **Dar es Salaam** umefanya vizuri kwa kukusanya kiasi cha **Shilingi Bilioni 83.86.** Mapato ya Mkoa huu yameongezeka kwa **Shilingi Bilioni 6.45** ukilinganisha na makusanyo ya Julai – Desemba, 2018. Mkoa wa mwisho katika wingi wa ukusanyaji wa mapato ni Mkoa wa **Katavi** ambao umekusanya **Shilingi bilioni 4.68** katika kipindi cha Julai hadi Desemba, 2019. Ingawa Mkoa huu umekuwa wa mwisho kwa wingi wa mapato, kuna ongezeko la **Shilingi Bilioni 2.3** ukilinganisha na mapato yaliyokusanywa Julai – Desemba, 2018, *(Jedwali Na. 3).*

## 2.3 Mapato ya Ndani ya Halmashauri kwa Kuzingatia Aina za Halmashauri kwa Kigezo cha Asilimia ya Makusanyo Ukilinganisha na Makisio

### 2.3.1 Halmashauri za Majiji

Katika kipindi hicho Halmashauri ya Jiji la **Dar es Salaam** imeongoza kundi la Halmashauri za Majiji kwa kukusanya mapato kwa **asilimia 71** ya makisio yake ya mwaka. Halmashauri ya Jiji la Dodoma imekuwa ya mwisho katika kundi hili ambapo imekusanya kwa **asilimia 41** ya makisio yake ya mwaka, *(Jedwali Na. 4(A)).*

### 2.4.2: Halmashauri za Manispaa

Halmashauri ya **Manispaa ya Ilemela** imeongoza kundi la Halmashauri za Manispaa ambayo imekusanya **asilimia 75** ya makisio yake. Katika kundi hili Halmashauri ya **Manispaa ya Kigoma** imekuwa ya mwisho ambapo imekusanya kwa **asilimia 26** ya makisio yake kwa Mwaka wa Fedha 2019/20 *(Jedwali Na. 4 (C)).*

### 2.4.3: Halmashauri za Miji

Kwa upande wa Halmashauri za Miji, Halmashauri ya Mji wa Njombe imeongoza kwa kukusanya kwa **asilimia 88** ya makisio ya mapato ya ndani kwa mwaka wa fedha 2019/20 ambapo Halmashauri ya Mji wa Babati imekuwa ya mwisho kwa kukusanya **asilimia 30** ya makisio ya mapato ya ndani kwa mwaka wa fedha 2019/*20 (Jedwali Na. 4(F)).*

### 2.4.4: Halmashauri za Wilaya

Aidha, kwa kundi la Halmashauri za Wilaya, Halmashauri za Wilaya za **Tunduru** na **Kibondo** zimeongoza kwa kukusanya **asilimia 104** ya makisio ya mapato ya ndani kwa mwaka wa Fedha 2019/20 wakati Halmashauri za Wilaya za **Mafia, Ukerewe na Gairo** zimekuwa za mwisho katika kundi hilo kwa kukusanya **asilimia 18** ya makisio ya mapato ya ndani kwa mwaka wa Fedha 2019/20, *(Jedwali Na. 4 (G)).*

## 2.5 **Mapato ya Ndani ya Halmashauri kwa Kuzingatia Aina za Halmashauri kwa Kigezo cha Wingi wa Makusanyo**

### 2.5.1 Halmashauri za Majiji

Katika kipindi hicho Halmashauri ya Jiji la **Dodoma** imeongoza kundi la Halmashauri za Majiji kwa kukusanya **Shilingi bilioni 29.75.** Halmashauri ya **Jiji la Dar es Salaam** imekuwa ya mwisho katika kundi hili ambapo imekusanya **Shilingi bilioni 6.03,** *(Jedwali Na. 4 (B)).*

### 2.5.2: Halmashauri za Manispaa

Kwa upande wa Halmashauri za **Manispaa ya Ilala** imeongoza kwa kukusanya **Shilingi bilioni 29.13**. Halmashauri ya **Manispaa ya Kigoma** imekuwa ya mwisho katika kundi hili ambapo imekusanya **Shilingi Milioni 694.93,** *(Jedwali Na. 4 (D)).*

### 2.5.3: Halmashauri za Miji

Katika kipindi hiki, Halmashauri ya **Mji wa Geita** imeongoza kwa wingi wa Mapato katika Halmashauri za Miji ambapo imekusanya **Shilingi Bilioni 4.64.** Halmashauri ya **Mji wa Nanyamba** imekuwa ya mwisho katika kundi hili ambapo imekusanya **Shilingi Milioni 459.44,** *(Jedwali Na. 4 (E)).*

### 2.5.4: Halmashauri za Wilaya

Halmashauri ya **Wilaya ya Chalinze** imeongoza kwa kukusanya mapato mengi kwa Halmashauri za Wilaya ambapo imekusanya **Shilingi Bilioni 3.89**. Halmashauri ya **Wilaya ya Bumbuli** imekuwa ya mwisho katika kundi hili ambapo imekusanya **Shilingi Milioni 186.08** *(Jedwali Na. 4 (H)).*

## 3.0 Matumizi ya Mapato ya Vyanzo vya Ndani ya Halmashauri

Katika kipindi cha Julai hadi Desemba, 2019 Halmashauri zimetumia kiasi cha **Shilingi Bilioni 228.48** ambayo ni **asilimia 64** ya mapato halisi yaliyokusanywa kuanzia Julai hadi Desemba, 2019. Kati ya matumizi hayo, **Shilingi Bilioni 137.56** zimetumika kwenye matumizi ya kawaida na **Shilingi Bilioni 90.92** zimetumika kwenye matumizi ya maendeleo. Aidha, katika kipindi hicho kiasi cha **Shilingi Bilioni 18.61** kimetumika kwenye miradi ya maendeleo ikiwa ni bakaa ya mapato ya ndani ya mwaka wa fedha 2018/19 ambayo ni **asilimia 54** ya bakaa yote (Shilingi Bilioni 34.33), hivyo kufanya jumla ya matumizi ya miradi ya maendeleo kufikia **Shilingi Bilioni 109.53**. Mchanganuo wa matumizi hayo ni kama unavyoonekana kwenye jedwali lifuatalo;-

| N/A | AINA YA MATUMIZI YA MAPATO YA NDANI | KIASI |
|---|---|---|
| 1 | Matumizi ya kawaida (Recurrent expenditure) | 137.56 |
| 2 | Matumizi ya miradi ya maendeleo (Development Expenditure) | 90.92 |
| | **Jumla Ndogo** | **228.48** |
| 3 | Matumizi ya Bakaa katika miradi ya maendeleo. | 18.61 |
| | **Jumla ya Matumizi yote** | **247.09** |

### 3.1 Matumizi ya Mapato ya Ndani Katika Miradi ya Maendeleo

Uchangiaji wa fedha za ndani katika shughuli za maendeleo umezigawa Halmashauri katika makundi makuu mawili. Kundi la kwanza ni Halmashauri zinazochangia asilimia 60 na kundi la pili ni Halmashauri zinazochangia asilimia 40 ya mapato ya ndani. Kama ilivyoelezwa hapo awali fedha zilizotumika katika miradi ya maendeleo kwa kipindi cha husika ni **Shilingi Bilioni 90.92.**

Uchambuzi wa taarifa hii unaonesha kuwa katika kundi la kwanza ambalo lina Halmashauri 16, Halmashauri ya **Mji wa Geita** imeongoza kwa kuchangia **asilimia 24** ya mapato halisi (own source proper) na Halmashauri ya **Manispaa ya Morogoro** imekuwa ya mwisho kwa kuchangia **asilimia 10** ya mapato halisi (own source proper).

Katika kundi la pili lenye Halmashauri 169, Halmashauri ya **Wilaya ya Kibondo** imeongoza kwa kuchangia **asilimia 36** ya mapato halisi (Own source proper) na Halmashauri ya mwisho katika kundi hili ni Halmashauri ya **Wilaya ya Morogoro** ambayo imechangia **asilimia 1** ya mapato halisi (own source proper). Aidha, Halmashauri nne za **Wilaya za Buhigwe, Kakonko, Handeni na Missenyi** hazijachangia kiasi chochote katika utekelezaji wa miradi ya maendeleo.

### 3.2 Matumizi ya Mapato ya Ndani Katika Mikopo ya Wanawake, Vijana na Watu Wenye Ulemavu.

Katika Kipindi cha Julai hadi Desemba, 2019 Halmashauri zilitoa Mikopo kiasi cha **Shilingi Bilioni 14.12** kwa Wanawake, Vijana na Watu Wenye Ulemavu ikiwa ni **asilimia 12** ya Bajeti ya Wanawake, Vijana na Watu Wenye Ulemavu ambayo ni **Shilingi Bilioni 62.36.**

Halmashauri nane zilizoongoza katika kutoa mikopo kwa Wanawake, Vijana na Watu Wenye Ulemavu ni Halmashauri za **Wilaya za Kibondo**, **Mlele**, **Mufindi**, **Mbarali** na **Njombe**, Halmashauri za **Manispaa za Ilala** na **Mpanda** na Halmashauri ya **Jiji la Dar es Salaam**. Halmashauri hizi zimechanga kati ya **asilimia 7** hadi **asimilia 10** ya mapato halisi (own source proper). Halmashauri za mwisho katika kutoa mikopo kwa Wanawake, Vijana na Watu Wenye Ulemavu ni Halmashauri ya **Jiji la Mwanza** na Halmashauri za **Miji Kibaha na Mafinga** ambazo zimechangia **asilimia 1** ya mapato halisi.

Hata hivyo, zipo **Halmashauri 37** ambazo hazijatoa kiasi chochote cha mikopo kwa Wanawake, Vijana na Watu Wenye Ulemavu kwa kipindi cha Julai hadi Desemba, 2019. Orodha ya Halmashuri hizo imeambatishwa, (*Jedwali Na. 6*).

## 4.0 Changamoto za Ukusanyaji Mapato ya Ndani kwenye Halmashauri kwa Kipindi cha Julai – Desemba, 2019.

Baadhi ya changamoto zilizojitokeza katika ukusanyaji wa mapato ya ndani kwa kipindi cha Julai – Desemba, 2019 ni pamoja na zifuatazo:

i. Makisio yasiyoakisi hali halisi ya mapato yanayoweza kukusanywa ambapo baadhi ya Halmashauri zimeweka makisio makubwa au madogo bila kuzingatia hali halisi ya uwezo wa vyanzo vya mapato ya ndani hivyo kushindwa kukusanya kufikia malengo au kuonekana zimekusanya zaidi.
ii. Baadhi ya Halmashauri hazisimamii kikamilifu matumizi ya mashine za kukusanyia mapato (POS);
iii. Kushindwa kuweka mikakati madhubuti ya kukusanya mapato kutoka kwenye vyanzo vipya vinavyobuniwa na Halmashauri;
iv. Matumizi yasiyo sahihi ya mifumo ya kielektroniki ambayo inasababisha kutopatikana kwa taarifa sahihi na kwa wakati; na
v. Kuwepo kwa baadhi ya Halmashauri ambazo hazizingatii utaratibu wa kufanya usuluhishi wa mapato kwenye mifumo ya kielekitroniki kwa wakati.

## 5.0 Mikakati ya Kutatua Changamoto

i. Mikoa inapaswa kuendelea kuzisimamia Halmashauri kutoa taarifa kupitia mifumo ya kielektroniki kwa kusisitiza kufanyika kwa usuluhisho wa taarifa katika mifumo mbalimbali na kusafisha takwimu chafu kwenye mfumo wa Epicor 10.2 ili kuwezesha kuwa na takwimu sahihi kwenye Dashboard ya mapato ya ndani;
ii. Ofisi ya Rais - TAMISEMI imeendelea kushirikiana na Wadau wengine katika kuzijengea uwezo Halmashauri kukusanya mapato ya ndani ikiwemo kuzinunulia Halmashauri mashine 7,227 za kukusanya mapato na kuwajengea uwezo wataalam wa fedha katika ngazi ya Mkoa; na
iii. Ofisi ya Rais TAMISEMI imeendelea kuandaa na kusimamia matumizi ya Miongozo mbalimbali ya usimamizi wa ukusanyaji wa mapato.

## 6.0 Hitimisho

Tunazipongeza Halmashauri zote zilizofanya vizuri katika kusimamia na kukusanya mapato ya ndani kwa kipindi hiki cha miezi sita (Julai, 2019 – Desemba, 2019). Aidha, Mikoa ambayo Halmashauri zake zimekusanya mapato chini ya asilimia hamsini (50%) hazina budi kufanya tathmini na kuhakikisha zinachukua hatua stahiki kuongeza mapato ya Halmashauri hizo ili kufikia malengo na bajeti za mapato ya ndani kabla ya mwisho wa Mwaka wa Fedha 2019/20.

Halmashauri zinahimizwa kuendelea kutumia kwa usahihi mifumo ya kielektroniki ya ukusanyaji wa mapato ya ndani na mifumo ya uhasibu ili kutoa taarifa kwa kufuata matakwa ya kisheria na kuzingatia viwango vya Kimataifa vya Uhasibu katika Sekta ya Umma (IPSAS). Ofisi ya Rais-TAMISEMI itaendelea kutangaza kwa umma taarifa za mapato ya ndani ya Halmashauri kila robo mwaka.

**Imetolewa na**



**Selemani S. Jafo (Mb)**

**Waziri wa Nchi, OR-TAMISEMI**
**09/02/2020**